# LUGHA, TUNGO NA MSAMIATI WA KISWAHILI

*Ahmed Sheikh Nabhany*

Natoa shukrani kwa wale mafundi ambao waliingia msituni wakakata miti na kuunda jahazi hili mpaka leo likawa lasafiri, na manahodha wakaweza leo kuniambia mimi kushika usukani ambao ni wa sehemu niijuayo nayo ni hii ya mashairi.

Ushairi, kwa jumla, ni tunguo. Unaposema tungo, unakusanya kila aina ya *utungo* wenye bahari mbalimbali. Na shairi ni bahari moja katika hizo. Sababu ya kuitwa utungo ni kuwa maneno utakayotumia yataka uyapange vizuri na yawe yenye kuvutia na kueleza kile unachokikusudia.

Bahari ya tungo ambayo ni maarufu sana siku hizi nì *mashairi. Shairi* lina mishororo (mistari) minne na kila mshororo una mizani 16; na mishororo yote huwa inafuatia mizani na vina. Mshairi hutunga *shairi* kwa lengo la kumfundisha mtu kitu fulani, kumfumba mtu (kama vile mshairi mwingine) au kwa kumwambia mtu jambo ambalo hawezi kumwambia usoni mwake moja kwa moja.

*Nyimbo* ni bahari nyingine inayotumiwa na ni utungo wenye mishororo mitatu yenye mizani12 (6-6 au 4-8) kila mshororo. *Nyimbo* zina mikondo yake na siku zote hutumiwa wakati wa sherehe fulani, kwa mfano, harusi ambapo watu huimba kuwaombea Mungu, bwana-arusi na bibi-arusi, au kumkaribisha mgeni. Pia hutumiwa kwa shauri ya mapenzi, kumvuta mtu kwa njia hii.

Bahari ya tatu ni *tenzi* ambazo ni tungo zenye mishororo 2 kila ubeti na kila mshororo una mizani 16. Mishororo 1½ ina kina kimoja na ½ ya mshororo wa pili kina chake ni tofa ıti. Utenzi aghalabu siku hizi hupangwa katika mishororo minne. Kila mshororo ukiwa na mizani 8, mishororo hii ikiwa katika kila kipande chake.

Tenzi zilikuwa zikitungwa toka zamani sana - na mpaka sasa zinaendelea kutungwa. Waandishi wa Kiswahili hapo zamani walikuwa hawaandiki vitabu kwa ajili ya kuhifadhi mambo mbalimbali bali walikuwa wakitunga tenzi kuhifadhi mambo hayo ili yawe sehemu ya historia ya wakati huo. Pia tenzi zilikuwa zikitumiwa kueleza historia ya mtu mashuhuri, mahali au tukio fulani.

Tenzi kwa kawaida huwa ndefu sana. Si jambo la kustaajabisha kuona utenzi una beti mpaka 1,000 au hata 1,500. Kwa mfano:
*Utenzi wa Mwana Kupona* (beti 102), *Utenzi wa Ngamia na Paa* (beti 384), *Utenzi wa Uhuru wa Kenya* (beti 858), *Utenzi wa Masaibu* (beti 1,070), *Utenzi wa Habibu* (beti 1,500) n.k.

Hebu sasa tumwangalie mshairi wa Kiswahili. Mshairi wa Kiswahili anapokusudia kutunga shairi huwa na kazi ngumu. Lazima achague maneno yake kwa uangalifu mkubwa na kuyapanga ili yalete mizani na vina katika vipande na beti zote za shairi lake. Na shairi lake liwe lamvutia msomaji ambaye kila akilisoma atake kuendelea mbele kwa ajili ya mvutio mkubwa uliomo ndani yake.

Mshairi kujua kupanga vina na mizani hajawa mshairi kamili bado. Lazima awe na ujuzi wa lugha yenyewe ya Kiswahili. Hiki ni kitu muhimu kwa mshairi. Na kupata lugha ya kutosha, mshairi lazima awe na ujuzi wa mambo mbalimbali. Kwa mfano, awe na ujuzi wa mambo ya bahari ambayo yana msamiati maalum wa kibahari. Pia ni jambo muhimu kwake kukusanya msamiati wa lugha ya kikale ambayo ilikuwa na ukwasi mkubwa. Hii aweza kupata kwa kuzisoma tenzi na tungo nyingine za watunzi wa zamani zilizohifadhiwa na ambazo zapatikana leo. Mfano mmoja wa utenzi wenye maneno kadha wa kadha ya zamani ni *Utenzi wa Fumo Liyongo* wa Mohamed Kijumwa (Mohamed Abubakar) wa Lamu. Fumo Liyongo mwenyewe alikuwa mshairi kwa upande wake. Alitunga utenzi wa beti 54 kumsifu mke wake toka utosini mpaka unyayoni. Tenzi hizi mbili ukizisoma na kuzifahamu, utapata msamiati wa faida kubwa — msamiati ambao haumo katika kamusi.

Ni maneno kama yapi ya kale ambayo leo hayatumiki au hayajulikani? Neno "dhahabu" (Kiarabu) kwa Kiswahili hasa ni *ng'andu* "Damu" (Kiarabu) ni ngeu na pia *mwinu* kwa kibantu. "Nafasi" (Kiarabu) maana yake ni *ngea*. Kwa mfano: "songea" maana yake "Nipishe kidogo nipate nafasi." Neno "nazi" ingawa ni la Kiswahili ni *ngole* kwa lugha ya wagema wa mnazi.

Kiswahili kina msamiati wa kutosha. Nasikitishwa na usemi wa baadhi ya watu kuwa Kiswahili ni lugha ambayo haijitoshelezi kwa upande wa msamiati. Mimi sikubaliani na dai hili. Naamini Kiswahili kina msamiati wa kutosha kama lugha nyinginezo kubwa za ulimwengu. Na ikiwa hakuna maneno ya kueleza mambo mapya yaliyozuka, Waswahili waweze kubuni maneno bila taabu. Hivyo ndivyo hapo kale Waswahili walivyokuwa wakikijenga Kiswahili kwa kubuni maneno mapya palipokuwa na haja ya kufanya hivyo. Kwa mfano: neno hili *ngamia* nini asili yake? Huyo mnyama *ngamia* alipoletwa huku mara ya kwanza Waswahili walipomwona hawakujua jina lake. Walimwona tu ana nundu na ni mnyama asiyeweza kubebeshwa mzigo wowote. Mtu mmoja akasema, "Mnyama huyu wa ajabu hana faida yoyote kwa sababu hawezi kubeba mzigo, lakini labda ataweza kubeba *ngaa miyaa*. Basi neno hili *ngamia* linatokana na kazi ya mnyama huyo.

Neno jingine la aina hii ni *risasi*. Waswahili walipojua kutengeneza "risasi" na kuitia katika bunduki wakaiita *kiandi-pota* kwa vile bunduki ikipigwa hutoa *kiandi* (cheche) na risasi pengine hutoka nyingi kwa pamoja, yaani *pota*.

Kwa upande wa elimu ya sayansi, jiografia na taaluma nyingine, wako baadhi ya watu wasemao kuwa Kiswahili hakijitoshelezi. Si kweli. Yako maneno ya Kiswahili ya kueleza mambo ambayo wengi wetu twayajua kwa Kiingereza tu na twadhani maana yake kwa Kiswahili hakuna. Neno "ray" kwa Kiswahili ni *uka* (kwa lafudhi ya Kiamu). Neno hili latokana na *kupambauka* (*kupambazuka* kwa Kimvita). Neno "image" ni *jazanda* kwa Kiswahili. "Mirage" kwa Kiswahili ni *mangati* (kutoka *mang'aa nti*: yaani 'kung'ara kwa nchi'); neno hili lilikuwepo toka zamani sana, si la hivi majuzi tu.

Pia twaweza kubuni maneno mapya ya Kiswahili kwa kuunganisha maneno mawili au zaidi itokeapo haja - na hapa napenda kusisitiza kuwa kazi hii hufanyika katika lugha zote. Mimi binafsi nimebuni maneno machache ambayo leo yakubaliwa na watu kadhaa. Nimebuni neno kutokana na maneno ya Kibantu *rununu* - "telephone" na *maninga* (macho).

Tukiendelea, napenda kusema kuwa leo sisi watu wa Kenya tuna lugha yetu wenyewe ya Kiswahili. Ni wajibu wa kila mmoja wetu kuishughulikia kwa kadiri ya uwezo wake, kukusanya maneno kutoka kwa wale ambao wana ujuzi na maarifa.

Twende kwa mtu yeyote ambaye twajua tutapata faida kubwa kwake. Kwa mfano, mvuvi, ingawa ni mtu mnyonge, aweza kutupa msamiati mkubwa sana wa kibahari ambao tunaweza kuutumia kufundishia wanafunzi.

Waandishi wa Kiswahili si watu waliozaliwa na kipawa cha lugha na ujuzi wa kuandika. La hasha; bali wao walikuwa ni watu waliokuwa wakijishughulisha sana kupata lugha ya kutosha kutoka kwa watu mbalimbali wenye ujuzi wa kazi mbalimbali.

Jambo jingine kuhusu lugha ya Kiswahili ni kuwa pengine maana ya baadhi ya maneno hubadilika baada ya kutumiwa kwa muda fulani. Kwa mfano, siku hizi twasikia watu wakisema, "mtu yule ni *bingwa* wa lugha." Neno hili *bingwa*, Waswahili hawampi mtu vivi hivi mpaka waridhike kabisa kuwa ana ujuzi kamili wa mambo fulani. Ni daraja ya juu sana. Neno *bingwa* maana yake yatokana na *kubingita,* yaani kubeba mizigo mingi kichwani, mgongoni na mingine -mikononi-na kuweza kwenda ingawa amelemezwa na uzito mkubwa. Mtu yule huitwa *mabinga.* Lakini leo *bingwa* ni mtu mwenye ujuzi wa kitu kimoja tu, kama vile bingwa wa lugha, bingwa wa kucheza mpira, bingwa wa kuunda jahazi na kadhalika. Maana ya *bingwa,* kwa hivyo, leo ni yenye kikomo kidogo tu.

Kila kazi au shughuli ya binadamu ina msamiati wake mahususi. Katika Kiswahili tuna msamiati wa ukulima, uvuvi, ugemaji wa minazi, ufugaji wa mifugo na kadhalika.

Basi mshairi wa Kiswahili atarajiwa awe na ujuzi wa maneno ya shughuli mbalimbali ili aweze kuitwa *bingwa* kwa kuwa tungo zake zina maana na ladha.

* - Hotuba iliyotolewa tarehe 6 Mei, 1977
katika Coast Girls' High School
kwenye Semina ya Fasihi ya Kiswahili
iliyotayarishwa na Kikao cha Walimu
wa Kiswahili wa Shule za Sekondari,
Mkoa wa Pwani, Mombasa.